*JARIDA LA CHALUFAKITA*
*Juz. 5, 2023, 80-92*

# MATUMIZI YA MSAMIATI KATIKA JAMIILUGHA YA WAFANYABIASHARA WA SOKO LA KARUME KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

Sauda Uba Juma
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
chudam017@gmail.com

**Ikisiri**

*Makala hii inalenga kubainisha msamiati maalumu wa Kiswahili unaoibuliwa na wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume jijini Dar es Salaam. Aidha, inalenga kuchunguza jinsi wafanyabiashara hao wanavyoutumia msamiati huo katika mchakato mzima wa kuendesha biashara zao katika miktadha mbalimbali. Utafiti huu, ni matokeo ya data za uwandani za usaili na ushuhudiaji. Data zingine zilipatikana maktabani kupitia usomaji wa nyaraka zinazoakisi mada hii kama vile: vitabu, tasnifu pamoja na majarida mbalimbali. Mbinu zote hizo kwa pamoja zimemsaidia mtafiti kupata data faafu zinazotosha kujibu lengo la makala hii. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo ya Fishman (1972) na data zimechanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Kwa ujumla, matokeo ya uchunguzi yameweka wazi msamiati fiche wa Kiswahili unaotumiwa na wafanyabiashara hao. Hivyo, tunapendekeza msamiati huo upitiwe na vyombo vilivyopewa dhamana ya kuunda istilahi, ili kuona namna bora ya kuweza kuusanifisha.*

**Maneno muhimu**: Msamiati, Jamiilugha, Wafanyabiashara

## 1.0 Utangulizi

Matumizi ya lugha ni dhana yenye mawanda mapana kwa kuwa dhana hii, inabeba mawasiliano ya jamii. Mawasiliano hayo, yanaweza kuwa ya muktadha wa mazungumzo au maandishi (Mbunda, 1996; Mekacha, 2011; Wanjala na Kivoi 2013). Eneo hili la matumizi ya lugha, limewahi kushughulikiwa na wanazuoni mbalimbali kwa wakati na malengo tofauti. Msanjila na wenzake (2011) wanaelezea kuwa kuna umuhimu wa kuchunguza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo kutokana na sababu zifuatazo: kwanza, kuwasaidia watumiaji wa lugha, kufahamu lugha gani waitumie katika miktadha rasmi na isiyorasmi. Pili, kunawasaidia wazungumzaji wa lugha kuelewa namna iliyo bora zaidi ya kuitumia lugha kulingana na miktadha mbalimbali baina ya mzungumzaji na msikilizaji.Tatu, kuchunguza tofauti za matumizi ya lugha kunawasaidia watumiaji wa lugha husika hususani wageni, kujua namna ya kuitumia lugha ngeni vizuri.

Wanaisimu hao pia wanatoa mifano ya maneno kama *daladala*, *matatu na kasheshe* ambayo awali yaliibuka kama misimu, sasa imekuwa sehemu ya msamiati wa Kiswahili na kuingizwa katika kamusi mbalimbali za Kiswahili. Hivyo, kwa ujumla kazi ya Msanjila na wenzake (khj) imetusaidia katika utafiti huu kwa kuwa, imetupata fununu juu ya masuala ya msingi ya matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Vilevile, kazi hiyo imetutia shauku ya kufanya utafiti uliozalisha makala hii ili kubaini msamiati mahususi unaotumiwa na jamii hiyo. Hivyo, matumizi ya msamiati tulioubaini kwa wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume, huenda kwa siku za baadaye ukasanifishwa na kukubalika kuwa msamiati rasmi wa Kiswahili na kuingizwa katika kamusi za Kiswahili.

Shayo (2015) alishughulikia semi zilizoandikwa katika maeneo ya biashara kama vile: magengeni, hotelini, migahawani na madukani. Katika utafiti wake huo alijikita zaidi kuangazia muundo, dhima na asili ya misimu. Utafiti wa Shayo (khj) umetupa uangavu wa kubaini misimu mbalimbali iliyoandikwa katika maeneo aliyoyashughulikia kama ambavyo tumeyabainisha. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa yeye alishughulikia misimu iliyoandikwa katika maeneo mbalimbali kwa ujumla wake. Pia, alishughulikia asili, dhima na muundo wa misimu katika maeneo yote hayo. Pamoja na juhudi aliyoifanya utafiti wake, haukushughulika na msamiati wanaoutumia wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume kwa lengo la kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Jambo ambalo limeshughulikiwa katika utafiti uliozalisha makala hii.

Juma (2016) alichunguza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo. Utafiti wake uliangazia zaidi mambo makuu matatu yanayozingatiwa na wazungumzaji wanapoitumia lugha katika miktadha ya mazungumzo. Mambo hayo ni mada ya mazungumzo, uhusiano wa wazungumzaji pamoja na mahali pa mazungumzo. Kazi ya Juma (khj) imetusaidia kubaini namna lugha inavyotumika kulingana na uhusiano, mada ya mazungumzo pamoja na miktadha mbalimbali ya mazungumzo. Hata hivyo, kazi ya Juma, haitupatii mifano halisi ya msamiati unaotumiwa katika muktadha mahususi wa mazungumzo. Hivyo basi, utafiti wake ni tofauti na utafiti uliozalisha makala hii ambao ulichunguza mifano ya msamiati na jinsi inavyotumiwa na wafanyabiashara katika muktadha mahususi wa mazungumzo.

Naye Adolph (2021) amefanya utafiti kuhusu aina mbalimbali ya misimu inayotumiwa na wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Katika utafiti wake amebainisha kuwa wanafunzi hao wanatumia misimu mbalimbali kama vile: *chabo, desa, jembe, kilaza, kipanga, tangopori na zimamoto, buku, jero, limetema, mawe, mpunga/mshiko* na *pambana na hali yako.* Aidha, Adolph (2023) amechunguza matumizi ya misimu miongoni mwa wanafunzi wa

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo amekijita kwa uwanja wa utani, soka na sanaa. Katika kazi zake hizo amependekeza kufanyika kwa tafiti zaidi katika uchunguzi wa misimu hasa ile inayoibuka katika miaka ya hivi karibuni. Mathalani, ufanyike utafiti juu ya misimu itokanayo na michezo, siasa, milipuko ya magonjwa na matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Tafiti za Adolph (khj), zimetusaidia kubaini msamiati maalumu ambao unatumiwa kama misimu na wanafuzi hao wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hata hivyo, tafiti zake zinatofautiana na utafiti uliozalisha makala hii, kwa kuwa yeye hakushughulikia msamiati wanaoutumia wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume kwenye harakati zao za biashara. Baada ya utangulizi huo, kipengele kinachofuata kinahusu mwega wa kinadharia uliotumika katika utafiti uliozalisha makala hii.

## 2.0 Mwega wa Kinadharia

Tafiti juu ya matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ikiwamo ya wafanyabiashara zinaweza kuongozwa na nadharia mbalimbali kama vile: Nadharia ya Diaglosia ya Ferguson (1959), Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo ya Fishman (1972), Nadharia Jumuishi ya Giles (1979) na Nadharia ya Makutano na Mwachano Giles (1982). Pamoja na kuwapo kwa nadharia mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya lugha, utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo. Nadharia hii imeonekana kuwa ni faafu zaidi kuliko nadharia zingine tulizozitaja kulingana na lengo la makala hii. Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo imeasisiwa na Fishman (1972). Fishman ni mwanaisimujamii ambaye alizaliwa mwaka 1926 huko Filadefia nchini Marekani. Mwanaisimu huyu anaelezea matumizi ya lugha yanaweza kubadilika kulingana na miktadha mbalimbali ya mazungumzo. Misingi ya nadharia hii ni: mosi kuchunguza jinsi muktadha wa kijamii na kitamaduni unavyoathiri matumizi ya lugha. Pili, kutilia mkazo umuhimu wa muktadha katika kuelewa mawasiliano ya lugha. Tatu, lugha haiwezi kuchunguzwa kipwekepweke, bali inapaswa kuchunguzwa katika muktadha wa kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kisiasa inamotumiwa.

Misingi hiyo imetumika na kutupa mwongoza kwa kuwa tumebaini kwamba, watumiaji wa lugha katika jamiilugha tunayoizungumzia, wana tabia ya kuchagua msamiati mahususi wa lugha kulingana na malengo yao. Kwa ujumla, Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo imesadifu barabara katika kuchambua data zinazohusiana na matumizi ya msamiati wa lugha kama ilivyojadiliwa katika makala hii. Pamoja na mwega wa kinadharia, sehemu inayofuata inahusu methodolojia iliyotumika katika ukusanyaji wa data za makala hii.

## 3.0 Methodolojia

Makala hii imetokana na utafiti wa uwandani uliofanyika katika Jiji la Dar es Salaam. Data zilikusanywa kuanzia mwezi Novemba hadi Desemba 2023. Eneo

lililohusishwa na utafiti huu ni soko la Karume lililopo katika Wilaya ya Ilala. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika kuipata sampuli ya watoataarifa 20 ambao ni wafanyabiashara waliohushwa na utafiti huu. Hivyo, sampuli iliyoteuliwa ilitosha kuwakilisha masoko ya wafanyabiashara wengine wanaouza viatu vya mtumba. Hii inatokana na ukweli kwamba sampuli haipaswi kuwa kubwa sana wala finyu sana bali inapaswa kuwa toshelevu (Sigh 2006; Garg na Kothari 2016). Aidha, data za makala hii zilipatikana kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji na usaili. Kupitia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti aliweza kuona jinsi wafanyabiashara hao wanavyoutamka na kuutumia msamiati huo kwa madhumuni maalumu. Vilevile, mbinu ya usaili ilitumika kwa wale tu wafanyabiashara wachache waliokusudiwa kwa minajili ya kutoa taarifa zilizohitajika katika utafiti huu. Data zilizokusanywa kupitia mbinu hizo kwa pamoja zilifanikisha kufikia lengo mahususi la makala hii. Aidha, mkabala wa kitaamuli katika kuchanganua data ulitumia. Hata hivyo, tumehusisha takwimu chache pale ilipotulazimu kufanya hivyo ili kuonesha idadi ya msamiati unaotokana na matumizi yao ya lugha katika biashara.

## 4.0 Matokeo

Kama ilivyodokezwa hapo awali kwamba makala hii inahusu matumizi ya msamiati kwa wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume. Matokeo yanaonesha kwamba wafanyabiashara hao wanautumia msamiati mahususi wa Kiswahili kwenye mchakato mzima wa kuuza na kununua bidhaa zao za viatu. Hata hivyo, wakati mwingine wafanyabiashara hao mbali na msamiati huo, huwa wanatumia pia miundo yenye maana tofauti na utaratibu wa lugha ya Kiswahili. Msamiati wote uliobainishwa katika makala hii, umepatikana kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji na usaili. Msamiati huo, umegawanywa katika vipengele tofauti kama ifuatavyo:

### 4.1 Msamiati Unaohusu Thamani ya Pesa

Kama tunavyofahamu kwamba katika suala zima la biashara pesa ndiyo kitu cha msingi. Hakuna biashara yoyote ile inayoweza kufanyika na kuendelea bila kuwa na mtaji wa pesa. Kwa msingi huo wafanyabiashara hao wameibua msamiati mwingi sana unaohusu thamani ya pesa. Kupitia mbinu ya ushuhudiaji, pamoja na usaili, tumebaini baadhi ya msamiati huo kama unavyofafanuliwa katika Jedwali Na. 1 lifuatalo:

**Jedwali Na. 1: Msamiati Unaohusu Thamani ya Pesa**

| Na. | Msamiati | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|
| *1.* | *Ganda* | *Shilingi elfu kumi* |
| *2.* | *Mizaliwa* | *Pesa* |
| *3.* | *Mzali* | *Shilingi mia tano* |
| *4.* | *Mbau* | *Shilingi elfu ishirini* |
| *5.* | *Mwisho wa mwezi* | *Shilingi elfu kumi na tano* |
| *6.* | *Namba mia* | *Shilingi elfu hamsini* |
| *7.* | *Kandoro* | *Shilingi elfu ishirini na tano* |
| *8.* | *Kifaru* | *Shilingi elfu tano* |
| *9.* | *Tembo* | *Shilingi elfu kumi* |
| *10.* | *Vitenente* | *Pesa za chenjichenji* |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Tukifuatilia mifano katika Jedwali Na. 1 hapo juu tunaweza kubaini msamiati kedekede unaotumiwa na wafanyabiashara ambao wanauza viatu vya mtumba katika soko la Karume. Aidha, tumebaini katika utafiti huu kwamba pesa ndiyo neno pekee lililopewa msamiati mahususi mwingi sana na wafanyabiashara hao. Mtafiti aliwahoji baadhi ya watoataarifa na kuwataka watoe sababu kuntu ambazo zinawafanya watumie msamiati teule mwingi mno kurejelea neno moja (pesa). Wafanyabiashara wote waliohojiwa walidai kwamba, msamiati huo umetokana na umuhimu wa pesa katika maisha ya binadamu. Kama anavyosema mtoataarifa mmoja:

> Pesa ndiyo sabuni ya roho. Hivyo inatakasa moyo mtu akiwa nayo moyo unafurahi na akiikosa moyo unahuzunika ndiyo maana baadhi ya watu wanaweza kufanya uhalifu wowote mradi wapate pesa.

Kauli hiyo iliyotolewa na mtoataarifa huyo inaakisi hali halisi ya maisha ya leo. Kila kitu kinahitaji pesa ndiyo maana kila uchao watu wanapambana kufanyakazi ili wapate pesa. Hivyo, tukirejelea katika Jedwali Na. 1 hapo juu tunaona kwamba maneno yote kuanzia la 1 hadi la 9 (maneno 9 kati ya 10) ambayo ni sawa na 90%, yanarejelea pesa za noti. Neno 1 tu kati ya maneno 10 sawa na 10% ndilo linarejelea pesa ndogondogo ambazo ni za chenji. Hii inatokana na ukweli kwamba, pesa za noti ndizo zinazopendwa zaidi na kila mtu. Pesa za chenji zinadharaulika kwa kuwa hazina matumizi makubwa. Hivyo, hata msamiati unaotumika ni wa kuzidunisha *vitenente*, ambapo *vi* inawakilisha udogo wake katika matumizi. Katika Jedwali hilohilo Na. 1, msamiati *mizaliwa* unaowakilisha pesa unaweza kufafanuliwa kwa upana zaidi kulingana na idadi ya pesa zilizokusudiwa. Mathalani: *Mizaliwa 10* sawa na shilingi *elfu 5.* Hivyo, wafanyabiashara hao wanaposema *mizaliwa 20*, *mizaliwa 70, mizaliwa 60, mizaliwa 90, mizaliwa 120* na *mizaliwa 200* huwa wanamaanisha

*shilingi elfu 10, shilingi elfu 35, shilingi elfu 30, shilingi elfu 45, shilingi elfu 60* na *shilingi laki moja*.

Licha ya maoni ya wanaisimu wengi kudai kuwa uhusiano baina ya leksia na kirejelewa ni wa kidhahania tu, kuna baadhi ya maneno katika lugha mbalimbali ambayo hudokeza uhusiano baina ya kiashiria na kiashiriwa. Kwa mujibu wa Matinde (2012), mbinu ambayo inadokeza uhusiano baina ya kitajwa na kirejelea ni ile ambayo hutumiwa kuunda maneno kwa kuzingatia uakisifu au uangavu wa kileksia, yaani hali ya leksia kuashiria au kudokeza kile kinachorejelea. Uangavu huo huweza kujitokeza katika hali zifuatazo: umbo la kirejelewa, sauti au mlio wa kirejelewa, tabia au sifa ya kirejelewa pamoja na athari ya kirejelewa. Hivyo, hali hiyo imeakisi baadhi ya msamiati ulioibuliwa na wafanyabiashara wa viatu vya mtumba katika soko la Karume kama unavyojidhihirisha katika Jedwali Na. 1 hapo juu. Kwa mfano, msamiati *kifaru (shilingi elfu 5)* na tembo *(shilingi elfu 10)* unarejelea pesa ambazo zina picha za wanyama hao. Hivyo uhusiano wa msamiati huo na maana zake sio wa kinasibu. Hii ni kwa sababu uhusiano huo umetokana na sifa fulani zilizomo kwenye pesa hizo. Vilevile *ganda, mizaliwa, mbau, mwisho wa mwezi* na *kandoro* ni msamiati ambao huenda umeibuliwa kinasibu tu.

### 4.2 Msamiati Unaorejelea Kukosa Pesa

Pamoja na msamiati unaohusu pesa, kuna msamiati mbalimbali unaorejelea hali ya kukosa pesa. Msamiati huu umekusanywa kupitia mbinu tulizokwisha kuzifafanua katika kipengele namba 4.0 hapo juu. Msamiati huo umeibuliwa na wafanyabiashara hao, kwa kuwa katika mchakato mzima wa kufanya biashara kuna kupata na kukosa. Inawezekana kabisa baadhi ya wakati mfanyabiashara akakosa faida na hata mtaji ukaisha. Hivyo, ni dhahiri kwamba mfanyabishara yeyote yule asitegemee kupata faida kila wakati anapouza biashara yake. Mara nyingine changamoto za kukosa kabisa pesa zinaweza kujitokeza. Msamiati unaohusu kukosa pesa unafafanuliwa katika Jedwali Na. 2 hapo chini:

**Jedwali Na. 2 Msamiati Unaorejelea Kukosa Pesa**

| Na. | Msamiati | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|
| *1.* | *Nina nondo* | *Sina pesa* |
| *2.* | *Nina vyuma* | *Sina pesa* |
| *3.* | *Sijatoa loki* | *Sijapata pesa* |
| *4.* | *Boksi gumu* | *Sijafanya kazi (sina pesa)* |
| *5.* | *Sina mizaliwa* | *Sina pesa* |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Tukichunguza mifano iliyomo katika Jedwaali Na. 2 hapo juu, tunaweza kugundua kwamba unarejelea vitu vigumu ambavyo sio rahisi kuvunjika kwa urahisi. Mara nyingine inalazimika itumike mashine au kitu kingine maalumu kinachoweza kukata

vitu vigumu kama vile *nondo* au *vyuma*. Kwa mantiki hiyo, msamiati *nina nondo, nina vyuma, sijatoa loki* na *boksi gumu* unarejelea hali ngumu ya kukosa pesa ambayo inamkabili mtu. Hivyo, kwa ujumla msamiati huo unawezekana umeibuliwa kutokana na ugumu wa kukata hivyo vitu vigumu, hali ambayo imelinganisha na ugumu ya kokosa pesa alionayo mhusika.

Kama ambavyo imedokezwa hapo awali kwamba kwa kawaida watumiaji wa lugha katika jamiilugha fulani mara nyingi, msamiati wanaouibua huwa wa kinasibu tu yaani hauna uhusiano wowote na maana ya kirejelewa na msamiati huo. Hata hivyo, baadhi ya msamiati wa kukosa pesa ulioibuliwa, una uhusiano wa moja kwa moja na maana inayorejelewa. Katika Jedwali hilo, imebainika msamiati kuanzia namba 1 hadi 4 kati ya 5 ambayo ni sawa na 80% huenda imeibuliwa na kuongozwa kwa vigezo maalumu. Msamiati wenye uangavu ni *nina nondo, nina vyuma, sijatoa loki* na *boksi gumu*. Msamiati huo umeibuliwa kutokana na uangavu wa sifa na tabia ya *nondo, vyuma na loki* ambavyo vina tabia ya ugumu wa kuvunjika. Aidha, msamiati 1 tu *(mizaliwa)* ambao ni sawa na 20% ndio ulioibuliwa kinasibu.

**4.3 Msamiati wa Kuomba Punguzo la Bei**

Kwa kawaida katika biashara yoyote iwayo kuna bei mahususi iliyowekwa na mfanyabiashara fulani kulingana na alivyonunua biashara hiyo. Wapo baadhi ya wafanyabiashara wanataka wapate faida kubwa katika biashara zao na wengine wanahitaji wapate faida japo ndogo tu, mradi wasiuze kwa bei ya hasara. Vyovyote iwavyo, kiuhalisia, mnunuzi naye wakati wote anaponunua bidhaa, huwa anataka ainunue kwa bei ya chini hasa pale anapoona anauziwa kwa bei ya juu sana. Aidha, kuomba punguzo la bei katika manunuzi haliwahusu wanunuzi wa nje peke yao. Suala hili linawagusa pia wafanyabiashara wadogo ambao wananunua viatu kutoka kwa wafanyabiashara wakubwa wanaofungua mizigo yao wenyewe. Kutokana hali hiyo, wafanyabiashara wa viatu vya mitumba katika soko la Karume wameibua msamiati mbalimbali unaohusu maombi hayo. Mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 3 inadhihirisha suala hilo:

**Jedwali Na. 3: Msamiati wa Kuomba Punguzo la Bei**

| Na. | Msamiati | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|
| *1.* | *Kumbomoa* | *Kumshusha bei* |
| *2.* | *Kumperembe* | *Kumrairai ili ashushe bei* |
| *3.* | *Kumpinda* | *kumlazimisha ashushe bei* |
| *4.* | *Kumlegeza/kumlaza* | *Kumlainisha ashushe bei* |
| *5.* | *Kumpetipeti* | *Kumpa maneno mazuri ili ashushe bei* |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Tukirejelea mifano iliyomo katika Jedwali Na. 3 hapo juu, tunaona kwamba kuna msamiati wa aina mbili. Mosi, kuna msamiati ambao unapatikana katika Kiswahili sanifu lakini unatofautiana kidogo kimaana na ule unaotumiwa na wafanyabiashara hao. Hata hivyo, maana katika Kiswahili sanifu na ile iliyokusudiwa na wafanyabiashara hao, huwa haziachani sana. Mathalani, maneno *kumbomoa, kumpinda* na *kumlegeza/kumlaza* yanakaribiana kimaana na ile maana inayotumika katika Kiswahili sanifu. Pili, baadhi ya msamiati unaotumiwa na wafanyabiashara hao umechipuka kutoka baadhi ya lahaja za Kiswahili au lugha nyingine za Kibantu. Kwa mfano, *kumperemba* msamiati huu umechipuka kutoka katika lahaja ya Kipemba. Tatu, kuna msamiati ambao huwa unaibuka tu kama misimu na hutumiwa na wanajamiilugha katika mazingira yao tofautitofauti kama wanavyoutumia wafanyabiashara hao, mathalani, *kumpetipeti*.

**4.4 Msamiati Unaohusu Wizi katika Biashara**

Mbali na msamiati utumikao kwa wanunuzi kuomba punguzo la bei kutoka kwa wafanyabiashara hao, kuna matumizi mingine ya msamiati ambao unahusu wizi anaofanyiwa mmiliki wa biashara. Kama ilivyo ada katika suala la kufanya biashara, mara nyingine mmiliki anaweza kutafuta mtu wa kumsaidia kwa nia njema kabisa. Lengo likiwa kupata msaada wa kuendesha biashara hiyo kwa makubaliano maalumu. Hali hii inaweza kuchanuzwa kutokana na mazingira tofautitofauti: mmiliki anaweza kuwa na biashara zaidi ya moja ambapo anashindwa kuzisimamia zote kwa wakati mmoja, kupata mapumziko kwa kupeana zamu baina ya mmiliki wa biashara na msaidizi wake. Pia, wakati mwingine mmiliki wa biashara hutingwa na majukumu mengine ya kikazi kama vile ya kuajiriwa na mtu binafsi au serikali pamoja na majukumu mengine ya kijamii kwa ujumla yanayomtanza mmiliki huyo. Baada ya makubaliano yao mchakato wa kusimamia biashara unaanza. Katika mchakato huo wa kuendesha biashara yanaweza kutokea mambo kadhaa ambayo huweza kusababisha biashara iyumbe.

Mosi, mmiliki wa biashara anaweza kukengeuka makubaliano waliyoyaweka baina yake na msaidizi wake. Pili, mmiliki kukosa busara na mahusiano mazuri na msaidizi wake. Tatu, kumtumikisha msaidizi wa biashara kama punda bila kujali utu. Nne, kukataa kumpatia msaidizi pesa yake kwa wakati au kukataa kumlipa kabisa kiasi cha fedha ambacho wamekubaliana. Vilevile, upande mwingine tatizo linaweza kutokea kwa msaidizi wa biashara na kusababisha biashara iyumbe. Msaidizi wa biashara anaweza kuikoroga biashara kwa makusudi kutokana na tamaa au kushawishiwa. Ushawishi huo unaweza kusababishwa na mfanyabiashara mwingine aliye jirani naye kwa kumpandikiza maneno ya fitina au choyo ili asiendelee kutoa msaada kwa mfanyabiashara huyo. Hivyo, mazingira kama hayo na mengine ambayo hatukuyataja hapo, ndiyo yanayoweza kuwafanya wafanyabiashara hao kuibua matumizi ya msamiati mbalimbali unaoakisi hali hiyo kama ifuatavyo katika Jedwali Na. 4:

**Jedwali Na. 4: Msamiati Unaohusu Wizi katika Biashara**

| Na. | Msamiati | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|
| *1.* | *Toa boko* | *Kaharibu kazi (kwa lengo la kuiba)* |
| *2.* | *Fuguta* | *Chukua usione huruma (kuiba sana)* |
| *3.* | *Toa kumvi/ meza/kwanyua* | *Iba* |
| *4.* | *Chocha* | *Chukua kidogo (usiibe sana)* |
| *5.* | *Gonga mbura* | *Chukua chako kabisa* |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Jedwali Na. 4 hapo juu linaonesha msamiati kadhaa ambao unatumiwa na baadhi ya wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume. Wafanyabiashara hao wanatumia maneno mbalimbali yenye maana mahususi. Maana hiyo huwa fiche ambayo si rahisi kueleweka kwa mtu wa kawaida anayezungumza Kiswahili. Kama tulivyotangulia kusema kuwa, maneno hayo yanayotumiwa mara nyingine huwa yanaibuka kutokana na vyanzo maalumu. Vyanzo hivyo vinaweza kuwa utani baina yao, kunasibisha sifa za mtu au kitu au mara nyingine kuwianisha msamiati wa lugha au lahaja fulani ambayo mtu ana umilisi nayo. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, matumizi ya msamiati mahususi kwa wanajamiilugha moja unaweza kuibuliwa na mtu mmoja tu na baadaye husambaa na kuenea kwa jamiilugha yote nzima. Utumiaji huo wa msamiati ulioibuliwa unasambaa na kuselea kimatumizi kwa jamiilugha hiyo.

Kwa mujibu wa data za ushuhudiaji na usaili za makala hii, zinaonesha kwamba kuna msamiati ulioibuka tu bila sababu, kwa mfano *toa boko na gonga mbura*. Aidha, kuna msamiati ambao kwa mujibu wa watoa taarifa, umeibuka kutokana na kuhusianisha sifa ya kitu kama vile *toa kumvi*. Msamiati huo umelinganishwa na jinsi nafaka kama mpunga inavyotenganishwa na pumba zake hadi kuwa mchele ambao uko safi kwa ajili ya kupikwa. Sifa kama hiyo imefananishwa na sifa ya mtu anayeibiwa na kuachwa mweupe kwa kuwa pesa zote huchukuliwa na aliyemuibia mfanyabiashara huyo. Ama maneno kama *fuguta, kwanyua* na *chocha* kwa mujibu ya watoa taarifa tuliowahoji, yamezuka kutoka katika lahaja ya Kiswahili (Kipemba). Hivyo, yumkini maneno hayo huenda yameibuliwa na mtu au watu fulani wanaoifahamu lahaja hiyo. Hatimaye, baadhi ya wafanyabiashara wengine wa soko hilo wakaendelea kuyatumia maneno hayo mpaka yalimezoeleka na kudumu katika matumizi yao ya kibiashara ya kila siku.

### 4.5 Msamiati Unayohusu Bei ya Viatu

Biashara yoyote ile iwayo inahusisha pande mbili yaani muuzaji na mnunuzi. Kila mfanyabiashara ana mbinu zake za kuuza biashara yake kutegemea na mazingira pamoja na taratibu alizojiwekea. Kwa upande wa baadhi ya wafanyabiashara

wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume, nao pia wana utaratibu wao wanaoutumia. Utaratibu huo huenda ndiyo unaowafanya wafanyabiashara hao, waibue msamiati mbalimbali ulio na matumizi tofauti katika Kiswahili. Katika soko la Karume, wafanyabiashara ya viatu wamegawanyika katika makundi makuu matatu. Kwanza, wafanyabiashara wenye msingi mkubwa wa fedha. Wafanyabiashara hao huwa wananunua viroba vya viatu kutoka kwa matajiri wanaoagiza mitumba mbalimbali kutoka nje. Pili, wafanyabiashara ambao wananunua viatu kutoka kwa wafanyabiashara wanaofungua viroba. Tatu, wanyabiashara ambao ni wapiga debe. Hawa mara nyingi huwa wanawauzia wale wafanyabiashara wanaofungua viroba. Katika hali kama hiyo, kuna msamiati mbalimbali unaohusu bei ambao unaibuliwa. Tufuatilie mifano iliyomo katika Jedwali Na. 5 hapo chini:

**Jedwali Na. 5: Misamiati Inayohusu Bei ya Viatu**

| Na. | Msamiati | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|
| *1.* | *Mwaga maji* | *Taja bei* |
| *2.* | *Maji yake?* | *Bei yake?* |
| *3.* | *Tandika* | *Uza kwa bei kubwa* |
| *4.* | *Karume Kisewe* | *Uza kwa bei ya juu* |
| *5.* | *Karume Kariakoo* | *Uza kwa bei ya chini* |
| *6.* | *Boksi gani?* | *Bei gani?* |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Katika Jedwali Na. 5 tunabaini matumizi mbalimbali ya msamiati unaotumiwa na wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume. Tukichunguza msamiati huo, tunagundua kwamba unahusu bei. Katika bei hizo za viatu, wakati mwingine wafanyabiashara hao wanatumia majina ya maeneo yaliyomo katika Jiji la Dar es Salaam. Majina hayo yanayotajwa yanaendana: ama na bei ya viatu kulingana na ubora wake au wakati mwingine endapo wafanyabiashara hao watagundua kwamba mnunuzi hana ulewa hata chembe kuhusu ubora wa viatu vya mtumba anavyotaka kununua. Data iliyomo katika Jedwali Na. 5, ambayo ilikusanywa kupitia njia ya ushuhudiaji na usali, inaonesha kwamba maneno 4 *(mwaga maji, maji yake, tandika na boksi gani)* kati ya 6 ambayo ni sawa na 67% yameibuliwa kinasibu tu, hayana uakisifu katika Kiswahili, lahaja zake au lugha za Kibantu. Maneno mawili *(Karume Kisewe na Karume Kariakoo)* ambayo ni sawa na 33% yana uangavu kuhusiana na bei zinazotolewa. Mathalani, muuzaji anapoambiwa na mwenye mali mpige *Karume Kisewe* ina maana amuuzie mnunuzi kwa bei ya juu. Vilevile, mwenye mali akisema *Karume Kariakoo* ina maana auze kwa bei ya chini.

Kwa mujibu wa watoa taarifa maneno hayo yameibuliwa kurejelea maeneo ya mahali kulingana na jiografia ya Dar es Salaam. *Karume Kisewe* ni maeneo yaliyoko mbali sana kijiografia wakati *Karume Kariakoo* ni maeneo yaliyoko jirani sana. *Karume* na *Kariakoo* ziko katika Wilaya ya Ilala, *Kisewe* iko katika Wilaya ya Temeke. Hivyo, wafanyabiashara hao wanaposema *Karume Kisewe* au *Karume Kariakoo* wanamaanisha ughali au urahisi wa bei kwa mnunuzi. Tulipojaribu kuwadodosa baadhi ya wafanyabiashara hao sababu zilizowafanya kuchagua maeneo hayo wakati kuna maeneo mengine mengi, walikosa majibu na kudai kwamba ndivyo wanavyotumia. Hii inaonesha kwamba pamoja na kuwa maneno hayo yana uangavu katika Kiswahili, hata hivyo yaliibuliwa kinasibu tu.

### 4.6 Msamiati Unaohusu Uzuri/Ubaya wa Viatu

Biashara ya mtumba ni ya kubahatisha na siku zote haina dhamana. Kuna wakati mfanyabiashara anaweza kupata mzigo mzuri unaoridhisha na wakati mwingine akapata mzigo ambao hauridhishi. Kwa vyovyote iwavyo, mfanyabiashara anahitaji kuuza biashara yake ili angalau arudishe pesa yake ya manunuzi kama sio kupata faida. Kwa mnasaba huo kuna matumizi mbalimbali ya msamiati unaohusu aina na ubora wa viatu unaoibuliwa na wafanyabiashara hao. Tutalii mifano katika Jedwali Na. 6 lifuatalo:

**Jedwali Na. 6: Msamiati Unayohusu Uzuri/Ubaya wa Viatu**

| **Na.** | **Msamiati** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|---|
| *1.* | *Mbegu* | viatu vizuri sana vinavyochaguliwa wakati mzigo unapofunguliwa |
| *2.* | *Muhogo* | Viatu visivyodumu vyenye soli inayoharibika haraka |
| *3.* | *Dai* | Viatu ambavyo sio vyeusi vinapakwa rangi nyeusi ili vionekane vyeusi |
| *4.* | *Mwatu/mafta* | Viatu vya mtumba ambavyo ni vizuri vinaonekana kama vipya kabisa |
| *5.* | *Ndaza* | Viatu vibaya vilivyobakia baada ya kuchaguliwa vilivyo vizuri |
| *6.* | *Mafua* | Viatu ambavyo sio halisi (original), maarufu vinaitwa vya Kichina |
| *7.* | *Vibungo* | Viatu vibaya |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Msamiati unaohusu aina ya viatu kama unavyojitokeza katika Jedwali Na. 6 unatumika kulingana na aina ya viatu alivyo navyo muuzaji. Msamiati huo mara nyingi unatumiwa na wafanyabiashara wanaofungua viroba na wanunuzi wa

rejereja. Kwa mfano, mfanyabiashara *anaposamini*[1] biashara yake ya viatu, anaweza kupata viatu vyenye ubora tofautitofauti. Hivyo matumizi ya maneno kama yanavyoonekana (taz. Jedwali Na. 6) huwa yanajitokeza. Neno *mbegu* kama tulivyofafanua kwenye upande wa tafsiri ya Kiswahili katika jedwali hilo hapo juu, linarejelea aina ya viatu vizuri na vyenye ubora wa hali ya juu. Kwa mujibu wa baadhi ya wafanyabiashara hao tuliowahoji, *mbegu* huchaguliwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kuja kuuzwa kwa bei ya juu siku za msimu wa biashara hiyo. Mathalani, siku za sikukuu au miezi ambayo shule zinakaribia kufunguliwa hasa kwa viatu vya shule.

Wafanyabiashara hao wanafanya hivyo kwa kuwa wanafahamu fika kwamba katika vipindi hivyo, biashara zao zitauzika vizuri na kwa bei ya juu ambayo itawapatia faida kubwa. Hivyo, msamiati *mbegu* kama unavyotumiwa na wafanyabiashara hao una, uangavu wa kisifa kwa kiasi fulani katika Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu katika Kiswahili, *mbegu*[2] wakati mwingine hutunzwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye, kulingana na msimu wa mazao husika. Aidha, *muhogo* limepewa uakisifu wa sifa ya muhogo kwamba unakatika kirahisi. Msamiati *dai* umetokana na rangi maalumu ambayo ukiipaka kwenye viatu ambavyo sio vyeusi vinabadilika na kuwa vyeusi. Neno *ndaza* kwa mujibu wa mtoa taarifa mmoja alidai kuwa, neno hilo nyumbani kwao anakotoka wanalitumia kwa maana ya machicha ya nazi ambayo yamebakia baada ya kuchujwa tui safi. Kwa mnasaba huo basi, neno hilo nalo huenda limetokana na uakisifu wa sifa ya viatu vibaya vilivyobakia baaada ya kuchaguliwa (kuchujwa) vilivyokuwa vizuri. Ama maneno *mwatu*, *mafta* na *vibungo* yameibuliwa kinasibu tu.

Kwa ujumla, Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo imefanikiwa kuchambua data zote zinazojitokeza katika Jedwali namba 1 mpaka 6. Majedwali hayo yamebainisha na kujadili msamiati unaohusu masuala mbalimbali ya kibiashara, yanayofanywa na wafanyabiashara waliolengwa katika utafiti huu. Kwa kutumia msamiati wao mahususi, wanajamiilugha hao, wanawasiliana na kuelewana kirahisi. Mawasiliano ya wanajamiilugha hao, yanafanikiwa kwa sababu wote wako katika muktadha wa aina moja wa kijamii na kitamaduni. Mazingira ya kijamii na kitamaduni yameshajengeka na kudumishwa miongoni mwao kiasi kwamba, yanawezesha kuwasiliana kwa kutuumia msamiati huo ili kufanikisha lengo lao la kibiashara kwa wepesi zaidi.

---

[1] Msamiati unaotumiwa na baadhi ya wafanyabiashara katika soko la Karume ambao unarejelea kuvipanga viatu vyenye ubora tofauti wakati anapofungua mzigo wake kwa mara ya kwanza.

[2] Nafaka, kijiti au mzizi ambao hupandwa ili kuchipua mmea wa jamii yake (BAKIZA 2010: 230)

**5.0 Mapendekezo na Hitimisho**

Katika makala hii tumechunguza matumizi ya msamiati unaotumiwa na wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume Jijini Dar es Salaam. Matokeo yameonesha kwamba wafanyabiashara hao, wanatumia msamiati mbalimbali mahususi katika mchakato mzima unaohusisha biashara yao. Ni ukweli usiopingika kwamba lugha si tuami. Hivyo, suala la kuibuka kwa msamiati maalumu kwa watu maalumu na muktadha maalumu halikwepeki. Hili ni suala la kawaida kwa jamii yoyote iwayo ulimwenguni kote. Kama inavyoelezwa na wanazuoni mbalimbali kwamba, kikundi kimoja cha watu wanapokaa katika mazingira ya aina moja wanaweza kuibua matumizi mbalimbali ya msamiati kwa minajili ya kukidhi haja yao. Hivyo, ni muhimu kuuchunguza msamiati huo ili uweze kueleweka bayana. Kwa kufanya hivyo, lugha inaweza kujiongezea ukwasi wa msamiati wake katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi, na kitaifa kwa ujumla. Jambo hili linaweza kutokea endapo tu msamiati huo utasanifishwa.

Uchunguzi huu vilevile, utazisaidia taasisi zilizopewa dhamana ya kuunda na kuzisanifisha istilahi mbalimbali za Kiswahili kama vile BAKITA na BAKIZA. Kwani kwa kawaida msamiati unaoundwa na taasisi hizo, huwa hautokei katika ombwe tupu bali unaweza kujuilikana kwa kushamiri matumizi yake katika jamii au kutokana na tafiti kama hizi. Hata hivyo, tafiti za kitaalamu ndizo zinazoweza kuibua mambo mengi na kuyaweka bayana ili yafahamike na kufanyiwa kazi na taasisi zinazohusika. Utafiti huu umejikita katika kushughulikia matumizi ya msamiati kwa wafanyabiashara wanaouza viatu vya mtumba katika soko la Karume. Utafiti mwingine mithili ya huu unaweza kufanyika kwa wafanyabiashara tofauti na mazingira tofauti ili tuwe na mahitimisho ya jumla kuhusu msamiati unaotumiwa na wafanyabiashara mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam.

**Marejeleo**

Adolph. E (2021). “Matumizi ya Misimu kwa Wazungumzaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu Nchini Tanzania: Uchunguzi Kifani wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere”. Katika *CHALUFAKITA,* Juz. 3: 156-173.

Adolph. E (2023). “Vyanzo vya Misimu Miongoni mwa Wanafunzi: Uchunguzi Kifani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam”. In *Journal of Kiswahili and Other African Languages,* Vol. 1 (1): 9-17.

BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Fishman, J. A (1972). *Language and Socialcultural Change: An Interdispciplinary Social Science Approach to Language in Society.* London: Newburg House Publishers.

Giles, H. (1979). “Ethnucity Markers in Speech”. In K.R. Scheres and Giles (eds). *Social Markers in Speech,* 251-289. London: University Press.

Giles, H. (1982). "An Intergroup Approach to Second Language Acquisition". *In Journal of Multilingual and Multicultural Development,* 3: 17- 40.

Juma, H. Kh. (2016). "Tofauti za Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali ya Mazungumzo". Katika *MULIKA*, Juz. 14: 12-23.

Garg, G. na Kothari, C.R. (2016). *Research Methodology: Methods and Techniques.* 3rd Edition New Delhi: New Age International Publishers.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mekacha, R. M. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Mbunda, F. L (1996) *Mbinu za Kufundisha Lugha ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam.

Msanjila, Y. P na Wenzake (2011), *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Sigh, J. K. (2006). *Fundamental of Research Methodology and Statistics*. New Delhi: New Age International Publishers.

Shayo, I. (2015). "Semi zilizoandikwa katika Maeneo ya Biashara": Uchunguzi kuhusu Asili, Muundo, Miktadha, na Utokeaji na Dhima". Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wanjala, F. & Kavoi, J. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundisha Kiswahili: Kwa Wanafunzi, Walifunzi na Walimu.* Mwanza: Serengeti Educational Puplishers.